

Chanjo ya Novavax COVID-19: Unachopaswa Kujua



Je, chanjo ya Novavax ni nini?

Chanjo mpya ya COVID-19 iliyoidhinishwa na Food and Drug Administration (FDA, Usimamizi wa Chakula na Dawa) Novavax, ni tofauti na chanjo nyingine za COVID-19 zinazopatikana Marekani kwa sasa. Novavax ni chanjo ya sehemu ndogo ya protini inayotumia teknolojia ileile iliyotumika kwa muda mrefu ambayo imeonakana katika chanjo nyingine zilizotumika sana kama vile HPV, homa ya ini B, na mafua. Novavax ni dozi ya awamu mbili, ambaop dozi ya pili inatolewa baada ya siku 21, inayopatikana kwa wale walio na miaka 12 na zaidi.

Novavax ni chanjo ya sehemu ndogo ya protini ya kiasili.

Ingawa kila chanjo iliyoidhinishwa infanya kazi ili kusaidia mfumo wetu wa kingamwili kutambua na kushambulia virusi vya COVID-19, Novavax hutumia teknolojia ya chanjo ya zamani inayofahamika sana.



- Chanjo za COVID-19 za sehemu ndogo ya protini zina vipande (protini) vya virusi vinavyosababisha COVID-19.
- Pia zina viungio pamoja na mafuta na sukari zinazokusudia kusaidia mfumo wa kingamwili kukabiliana na virusi na kukulinda siku zijazo.
- Hazina mRNA

Madhara ya baada ya kutumia Novavax yanaonekana kuwa madogo.

Madhara ya muda mfupi ya kutumia Novavax si kama madhara ya kawaida yanayoonekana kwenye chanjo nyingine za COVID-19. Maumivu/ulaini, wekundu na kuvimba kwenye sehemu ambapo sindano ilidungwa, na pia uchovu, maumivu ya misuli, maumivu ya kichwa, maumivu ya viungo, kichefuchefu/kutapika na homa. Chanjo za COVID-19 za sehemu ndogo ya protini haziwezi kusababisha COVID-19 wala magonjwa mengine.

Je, data inaonyesha nini?

Tafiti za majaribio ya matibabu zilizofanywa katika majira ya kuchipua ya 2021 zilionyesha kwamba chanjo ya Novavax ilionyesha ufanisi wa asilimia 90 dhidi ya kuzuia maambukizi ya COVID-19 na ufanisi wa asilimia 100 kuzuia vifo vinavyohusiana na COVID-19.

Chanjo inasemekana kuchochea mikabiliano mipana ya kingamwili dhidi ya vibadala vyote vya COVID-19, ikiwemo BA.5, kulingana na majaribio yanayoendelea. Chanjo za sehemu ndogo kama vile Novavax hazitumii virusi vyovyote hai na haziwezi kubadilisha wala kuathiri jeni zetu. Pia tumejifunza kwamba Novavax:



- Imetumiwa kwa ufanisi katika nchi nyingine nyingi, ikiwemo Kanada, tangu 2021
- Haina viambato vinavyotumika katika chanjo nyingine vinavyosababisha mizio
- Hutumia teknolojia ileile inayojulikana katika chanjo maarufu kama vile mafua, HPV, homa ya ini B na ugonjwa wa vipete

Novavax imepitia mchakato wa FDA Emergency Use Authorization (EUA, Idhini ya Matumizi ya Dharura) na ni chaguo sahihi haswa kwa wale wanaotafuta mbadala wa [chanjo za mRNA](#).

Dozi za ziada kwa vikundi vingine zinaweza kupendekezwa katika siku za baadaye.

Chanjo bado ni chaguo bora zaidi.

COVID-19 inapoendelea, machaguo zaidi ya chanjo yamepatikana. Ni muhimu kukumbuka kwamba kuchanjwa ni bora. Haijalishi chapa ya chanjo, kupata chanjo ni kinga yako bora dhidi ya COVID-19 na madhara yake. Zungumza na mtoa huduma wako kuhusu chaguo linalokufaa zaidi.